JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

# MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA JINSIA NA MAENDELEO YA WANAWAKE YA MWAKA (2023)

**2023 – 2033**

## YALIYOMO

**SURA YA KWANZA ........ 2**
**USULI ........ 2**
1.1 Utangulizi ........ 2
1.2 Masuala ya Kisera ........ 3
1.3 Mgawanyo wa Majukumu ya Wadau ........ 3
1.4 Matokeo Yanayotarajiwa kutokana na Utekelezaji wa Mkakati wa Sera ........ 4
1.5 Mpangilio wa Mkakati ........ 4
**SURA YA PILI ........ 5**
**DIRA, DHIMA NA MALENGO YA SERA ........ 5**
2.0 Utangulizi ........ 5
2.1 Dira ........ 5
2.2 Dhima ........ 5
2.3 Malengo ya Mkakati ........ 5
2.3.1 Lengo Kuu ........ 5
2.3.2 Malengo Mahsusi ........ 5
**SURA YA TATU ........ 7**
**MALENGO, MIKAKATI NA SHABAHA ........ 7**
3.1 Utangulizi ........ 7
3.2 Maeneo ya Sera ........ 7
3.2.1 Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ........ 7
3.2.2 Ukatili wa Kijinsia ........ 8
3.2.3 Haki na Usawa wa Kiuchumi ........ 9
3.2.4 Jinsia , Uongozi na Maamuzi ........ 10
3.2.5 Jinsia, Elimu na Mafunzo ........ 10
3.2.6 Afya na Jinsia ........ 11
3.2.7 Jinsia, Teknolojia na Ubunifu ........ 12
3.2.8 Jinsia na Takwimu ........ 13
3.2.9 Wanawake, Amani na Usalama ........ 14
3.2.10 Jinsia na Utawala Bora ........ 15
3.2.11 Jinsia na VVU na Ukimwi ........ 16
3.2.12 Jinsia na Mazingira ........ 16
**SURA YA NNE ........ 18**
**UFUATILIAJI NA TATHMINI ........ 18**
4.1 Utangulizi ........ 18
4.2 Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ........ 19
4.3 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ........ 19
4.4 Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini ........ 20
4.4.1 Mawanda ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ........ 20
4.4.2 Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini ........ 20
4.5 Mpango wa utoaji taarifa ya utendaji kazi ........ 20
4.5.1 Mpango wa Taarifa ya Ndani ........ 20
4.5.2 Mpango wa Utoaji wa Taarifa kwa Wadau wa Nje ya Wizara ........ 21
4.5.3 Matumizi ya taarifa za Ufuatiliaji na Tathimini. ........ 21
**KIAMBATISHO 1: ........ 21**
**BANGO KITITA LA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA SERA YA TAIFA YA JINSIA NA MAENDELEO YA WANAWAKE (2023) ........ 21**

## SURA YA KWANZA

## USULI

### 1.1 Utangulizi

Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023) ni matokeo ya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000) ambayo ilibaini mafanikio yaliyofikiwa pamoja na changamoto zinazopaswa kushughulikiwa. Mafanikio yaliyoonekana katika mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000) ni pamoja na: Kupungua kwa matukio ya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto; Kuundwa kwa programu za kuwawezesha wanawake kiuchumi; Kuundwa kwa Madawati ya Jinsia katika ngazi za Wizara, Idara, Wakala, Mashirika, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Vituo vya Polisi, Maeneo ya Umma na Taasisi za Elimu ya Juu; Kuhamasisha kutungwa kwa sheria zinazozingatia Usawa wa Jinsia; Mapitio ya sheria zenye ubaguzi wa kijinsi; Kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa wanawake hususan huduma ya afya ya uzazi na kuongeza idadi ya udahili wa wasichana na wavulana katika shule za msingi na sekondari kwa uwiano wa 1:1.

Pamoja na mafanikio hayo, zipo changamoto zilizobainishwa. Changamoto hizo ni pamoja na: Ushiriki mdogo wa wanaume katika juhudi za kukuza usawa wa jinsia; Kuendelea kuwepo kwa matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia; Kuendelea kuwepo kwa mila na desturi zinazowanyima wanawake fursa ya kumiliki rasilimali za uzalishaji; Mila na Desturi zenye madhara zinazosababisha vifo vinavyotokana na uzazi na kuongezeka kwa majukumu ya wanawake kutokana na upatikanaji mdogo wa huduma za maji, nishati na ufikiwaji mdogo wa huduma za Hifadhi ya jamii kwa wanawake na wanaume waliopo katika sekta isiyo rasmi.

Kwa zaidi ya miongo miwili, Zera (2000) ilitoa mwongozo kwa wadau kuhusu utekelezaji wa mipango mbalimbali iliyolenga kukabiliana na changamoto zinazozuia mafanikio ya kukuza usawa wa jinsia. Hata hivyo, taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Sera (2000) ilibainisha mapungufu, changamoto na masuala mapya yaliyojitokeza. Hali hiyo ilisababisha kufanyika kwa mapitio na kuandaliwa kwa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023). Upungufu uliobainishwa ni pamoja na: Sera kutojumuisha aina nyingine za ukatili wa kijinsia hususan ukatili

kwa njia ya TEHAMA katika mitandao ya kijamii, ukatili wa kimwili na kingono kwenye Taasisi za Elimu; kutokuwepo kwa msukumo wa uzingatiwaji wa masuala ya jinsia na afya hususan uhimizaji wa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana kuwa na utamaduni wa kupima afya mara kwa mara ikiwemo magonjwa ya saratani ya shingo ya kizazi, matiti na tezi dume; ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama; Jinsia na huduma za kidijitali. Vilevile, Sera haikuzingatia masuala mtambuka ikiwemo Jinsia na Utawala Bora na VVU/UKIMWI hivyo kukosa matamko ya kisera.

Aidha, Ili kutekeleza Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023) Wizara imeandaa Mkakati wa Utekelezaji wa 2023 - 2033. Mkakati huu unatoa mwelekeo wa utekelezaji wa malengo ya sera kwa kubainisha mikakati, malengo, viashiria, makadirio ya bajeti, ufuatiliaji, tathmini na mpango wa utoaji wa taarifa ya utekelezaji wa sera.

### 1.2 Masuala ya Kisera

Mkakati huu wa utekelezaji unajumuisha maeneo muhimu ya Sera kama yalivyoonyeshwa katika Sera (2023). Maeneo hayo ni pamoja na: Uwezdshaji wa Wanawake Kiuchumi; Ukatili wa Kijinsia; Haki na Usawa wa Kiuchumi; Jinsia, Uongozi na Maamuzi; Jinsia, Elimu na Mafunzo; Jinsia na Afya; Jinsia, Teknolojia na Ubunifu; Takwimu za Kijinsia; Wanawake, Amani na Usalama. Pia, mkakati unajumuisha masuala mtambuka ambayo ni Jinsia na Mazingira; Jinsia na Utawala Bora na Jinsia na UKIMWI.

### 1.3 Mgawanyo wa Majukumu ya Wadau

Mkakati huu wa utekelezaji unahitaji juhudi za pamoja katika utekelezaji wa Sera (2023) kutoka katika ngazi za Taifa, Kanda na kimataifa ili kufikia Malengo ya Sera.Miongoni mwa wadau watakao husika katika kutekeleza Sera ni pamoja na: - Wizara yenye Dhamana na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalu; Wizara yenye Dhamana na Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu; Wizara yenye Dhamana na Fedha; Wizara yenye Dhamana na Mazingira; Wizara yenye Dhamana na Maji; Wizara yenye Dhamana na Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Wizara yenye Dhamana na Ardhi; Wizara yenye Dhamana na Kilimo; Wizara yenye Dhamana na Mifugo na Uvuvi; Wizara yenye Dhamana na Michezo; Wizara yenye Dhamana ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara yenye

Dhamana na Katiba na Sheria; Wizara yenye Dhamana na Ulinzi na Usalama; Wizara yenye Dhamana na Ujenzi; Wizara yenye Dhamana na Uchukuzi; Wizara yenye Dhamana na Nishati; Wizara yenye Dhamana na Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara yenye Dhamana na Uwekezaji na Mipango; Wizara yenye Dhamana na Viwanda na Biashara; Wizara yenye Dhamana na Utumishi na Utawala Bora; Wizara yenye dhamana na Madini; Wizara yenye dhamana ya Afya; Wizara yenye Dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Sekretarieti za Mikoa; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Bunge; Asasi za Kiraia/Bodi za Kitaalam; Sekta Binafsi; Taasisi za Elimu na Utafiti; Wadau wa Maendeleo; Vyombo vya Habari; Familia na Jamii.

## 1.4 Matokeo Yanayotarajiwa kutokana na Utekelezaji wa Mkakati wa Sera

Utekelezaji wa mkakati huu utawezesha kufikia malengo tarajiwa ya Sera (2023) kwa kujenga mazingira ya utekelezaji yanayohimiza juhudi za kuboresha usawa wa kijinsia kama haki msingi ya binadamu. Aidha, Mkakati huu utaweka mifumo muhimu ya kuimarisha utekelezaji na ufuatiliaji wa Sera, Sheria na Miongozo inayolenga kuendeleza usawa wa kijinsia; Vilevile, utasaidia kupunguza tofauti za kijinsia zilizopo baina ya wanawake na wanaume na kusaidia kuwawezesha wanawake, wasichana, wanaume na wavulana kutumia uwezo wao kamili wa kibinadamu ili kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

## 1.5 Mpangilio wa Mkakati

Mkakati huu wa utekelezaji una Sura nne kwa mpangilio ufuatao; Sura ya kwanza inaonyesha Maelezo ya Utangulizi kuhusu Mkakati wa Utekelezaji wa Sera (NGWDP (2023); Sura ya pili inaonyesha Dira, Dhiman na Malengo ya Sera. Aidha, Sura ya tatu inabainisha Mikakati ya utekelezaji; na Sura ya nne inaeleza Mfumo wa ufuatiliaji, utoaji taarifa na tathmini.

# SURA YA PILI

# DIRA, DHIMA NA MALENGO YA SERA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inatoa maelezo kuhusu Dira, Dhima na Malengo ya Mkakati wa utekelezaji wa Sera kwa kipindi cha 2023 - 2033.

## 2.1 Dira

Nchi yenye usawa na haki wa kijinsia ambapo wanawake na wanaume wanaishi kwa pamoja na kufaidika kwa usawa kutokana na fursa zilizopo za kijamii na kiuchumi.

## 2.2 Dhima

Kukuza usawa wa kijinsia katika nyanja zote za maisha na maendeleo ikiwa ni pamoja na nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni kupitia maendeleo na utekelezaji wa sera, mikakati, programu, miradi na mipango inayozingatia na kulinda ustawi wa wanawake na wanaume; wavulana na wasichana na kuimarisha ukuaji na maendeleo ya uchumi wa taifa.

## 2.3 Malengo ya Mkakati

### 2.3.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la Mkakati huu ni kuweka afua za kimkakati za kutekeleza matamko ya Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023.

### 2.3.2 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023 ni kama ifuatavyo: -

(i) Kukuza usawa wa kijinsia katika upatikanaji wa fursa za kiuchumi na kifedha kwa wanawake na wanaume;

(ii) Kutokomeza aina zote za ukatili wa kijinsia ikiwemo ukatili wa kijinsia mitandaoni;

(iii) Kuwa na jamii inayoheshimu usawa na haki kwa wote;

(iv) Kuweka mazingira wezeshi kwa wanawake ili kushiriki kikamilifu katika ngazi zote za uongozi na maamuzi;

(v) Kukuza usawa wa kijinsia katika upatikanaji wa elimu bora na mafunzo;

(vi) Kuhimiza huduma za afya jumuishi zikiwemo afya ya uzazi na magonjwa yasiyoambukizwa kwa wanawake na wanaume;

(vii) Kuongeza matumizi ya nishati safi kwa wanawake na wanaume mijini na vijijini

(viii) Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika uwezeshaji wa wanawake;

(ix) Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji, utunzaji na utumiaji wa takwimu za kijinsia;

(x) Kuzingatia masuala ya kijinsia katika mifumo na programu za amani na usalama;

(xi) Kuhamasisha misingi ya utawala bora inayozingatia masuala ya kijinsia.;

(xii) Kuhimiza uzingatiaji wa huduma kwa Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI pamoja na kujikinga na maambukizi mapya ya VVU kwa wanaume na wanawake; na

(xiii) Kukuza uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika usimamizi wa mazingira.

# SURA YA TATU

# MALENGO, MIKAKATI NA SHABAHA

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inatoa mikakati ya kimkakati ya kushughulikia masuala muhimu ya jinsia na maendeleo ya wanawake kama yalivyoelezwa katika Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023). Mkakati huu unatoa mwongozo wa utekelezaji wa Sera kwa kueleza malengo mahusus ya sera, mikakati ya utekelezaji, na shabaha zitakazofikiwa wakati wa utekelezaji (2023 - 2033).

## 3.2 Maeneo ya Sera

### 3.2.1 Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi

**Lengo**

Kuimarisha usawa wa kjinsia katika upatikanaji wa fursa za kiuchumi na mitaji kwa wanawake na wanaume.

**Mikakati**

(i) Kuchukua hatua za kupunguza mkwamo na kupanua upatikanaji wa rasilimali za mitaji kwa wanawake ili kuongeza uzalishaji;

(ii) Kubainisha na kutekeleza jitihada zenye lengo la kuwawezesha wanaume na wanawake kutambua na kutumia fursa za kiuchumi;

(iii) Kushawishi kuzingatiwa kwa mgawanyo na upangaji wa majukumu ya kazi za nyumbani na majukumu ya malezi kati ya wanaume na wanawake kwa kuzingatia usawa;

(iv) Kuendeleza na kuimarisha ushiriki wa wadau katika kusaidia kufanya mabadiliko ya kijamii yenye maadili chanya;

(v) Kuhimiza umuhimu wa kujiunga katika programu za hifadhi ya jamii kwa wanawake na wanaume, wafanyakazi wa sekta binafsi na sekta za umma wanaoishi mijini na vijijini.

**Shabaha**

(i) Kuhakikisha ongezeko la wanawake wanaopata mitaji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi ifikapo Juni, 2033;

(ii) Jitihada za kuwezesha wanaume na wanawake kutambua na kuendeleza fursa za kiuchumi ifikapo Juni 2033;

(iii) Jitihada za kuwezesha wanaume na wanawake kutambua na kutekeleza fursa za kiuchumi ifikapo Juni, 2033;

(iv) Kuwepo kwa mgawanyo sawa wa majukumu ya kazi za nyumbani na malezi kati ya wanaume na wanawake ifikapo Juni, 2033;

(v) Ushirikishwaji wa wadau katika kukuza mabadiliko chanya ya mila na maadili ya kijamii kuimarishwa ifikapo Juni, 2033; na

(vi) Upatikanaji na usambazaji wa huduma za usalama wa jamii kwa wafanyakazi katika sekta binafsi na sekta za umma kwa wanawake na wanaume wanaoishi mijini na vijijini kuimarishwa ifikapo Juni, 2033.

### 3.2.2 Ukatili wa Kijinsia

**Lengo**

Kutokomeza aina zote za ukatili wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na ukatili wa kijinsia mtandaoni.

**Mikakati**

**(i)** Kuandaa programu za kuongeza uelewa mtandaoni kuhusu kuzuia na kushughulikia ukatili wa kijinsia mtandaoni;

(ii) Kuimarisha mifumo ya uratibu kwa ajili ya kuzuia na kushughulikia ukatili wa kijinsia katika jamii;

(iii) Kuanzisha mifumo ya kuzuia na kushughulikia ukatili wa kijinsia katika jamii;

(iv) Kuandaa na kutekeleza programu za kuongeza uelewa kuhusu masuala masula ya jinsia na malezi chanya;

(v) Kuamasisha ushiriki wa vikundi vya wanaume, taasisi za dini na mashirika yasiyo ya kiserikali katika programu za kuzuia ukatili wa kijinsia.

**Shabaha**

**(i)** Matukio ya ukatili wa kijinsia kupungua ifikapo 2033;

**(ii)** Mifumo ya uratibu kwa ajili ya kuzuia na kushughulikia ukatili wa kijinsia katika jamii kuimarishwa ifikapo 2033;

**(iii)** Vikundi vya kijamii vya kudhibiti ukatili wa kijinsia kulingana na jamii kuanzishwa ifikapo 2033;

**(iv)** Kampeni za kuongeza uelewa kuhusu masuala ya malezi chanya yenye kuzingatia jinsia zimetekelezwa ifikapo 2033;

**(v)** Kampeni za kuongeza uelewa kuhusu mazoea chanya ya malezi yenye kuzingatia jinsia zinatekelezwa ifikapo 2033; na

**(vi)** Ushiriki wa vikundi vya wanaume, taasisi za dini na mashirika yasiyo ya kiserikali katika jitihada za kuzuia ukatili wa kijinsia vimewezeshwa ifikapo 2033.

### 3.2.3 Haki na Usawa wa Kiuchumi

**Lengo**

Kuhimiza uzingatiaji wa haki na usawa wa kiuchumi kwa Wanawake na Wanaume katika jamii.

**Mikakati**

(i) Kuimarisha uwekezaji katika miundombinu inayopunguza mzigo wa kazi kwa wanawake na wasichana (Vituo vya kulea watoto mchana, vituo vya elimu ya awali na makuzi, huduma za maji na nishati);

(ii) Kusimamia utekelezaji wa mifumo ya kisheria inayoendeleza upatikanaji na usimamizi wa rasilimali za uzalishaji kwa wanawake;

(iii) Kuimarisha utekelezaji wa mipango ya kazi bora kwa wanawake na wanaume katika sekta rasmi na isiyo rasmi;

(iv) Kukuza uwekezaji katika utafiti na maendeleo kuhusu haki na haki za kiuchumi kwa wanawake;

(v) Kuandaa na kutekeleza programu za mafunzo ya ujumuishwaji wa masuala ya kijinsia katika mipango ya kiuchumi na kifedha.

**Shabaha**

(i) Mzigo wa kazi zisizolipwa kwa wanawake na wasichana kupunguzwa ifikapo 2033;

(ii) Utekelezaji wa mifumo ya kisheria inayoendeleza upatikanaji wa udhibiti wa rasilimali za uzalishaji kwa wanawake kusimamiwa ifikapo 2033;

(iii) Uwekezaji katika tafiti za maendeleo kuhusu haki na haki za kiuchumi za wanawake kukuza ifikapo 2033;

(iv) Kazi bora kwa wanawake na wanaume kuongezeka katika sekta rasmi na isiyo rasmi ifikapo 2033;

(v) Programu za kuimarisha uwezo wa kuzingatia uingizaji wa masuala ya jinsia katika mipango ya kiuchumi na kifedha kuandaliwa ifikapo 2033; na

(vi) Programu za kuimarisha uwezo wa uingizaji wa masuala ya jinsia katika mipango ya kiuchumi na kifedha kutekelezwa ifikapo 2033.

### 3.2.4 Jinsia , Uongozi na Maamuzi

**Lengo**

Kuweka mazingira wezeshi kwa wanawake kushiriki kikamilifu katika ngazi zote za uongozi na maamuzi.

**Mikakati**

i. Kuhamasisha ushiriki wa wanawake, wanaume, wasichana, na wavulana katika ngazi zote za uongozi na maamuzi; na
ii. Kundaa programu za kuongeza uelewa kuhusu ushiriki wa wanawake katika uongozi na maamuzi.

**Shabaha**

i. Ushiriki wa 50:50 katika ngazi zote za uongozi na maamuzi kufikiwa ifikapo 2033;
ii. Programu za kuongeza uelewa kuhusu ushiriki wa wanawake katika uongozi na maamuzi zimeandaliwa ifikapo 2033; na
iii. Programu za kuongeza uelewa kuhusu ushiriki wa wanawake katika uongozi na maamuzi kutekelezwa ifikapo 2033.

### 3.2.5 Jinsia, Elimu na Mafunzo

**Lengo**

Kuhimiza usawa wa kijinsia katika upatikanaji wa elimu bora na mafunzo.

**Mikakati**

i. Kundaa programu za kuongeza uelewa katika jamii za kuhimiza ushiriki wa wanawake na wasichana katika programu za elimu katika ngazi zote;
ii. Kuimarisha miundombinu rafiki na vifaa vya elimu vinavyoweza kutumika kwa wavulana na wasichana;
iii. Kuwezesha ushiriki wa wasichana katika programu za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM);

iv. Kuandaa na kutekeleza afua shirikishi za kusaidia kuongeza idadi ya uandikishwaji wa wasichana na wavulana na kuhakikisha wanabakia shuleni na;
v. Kundaa mtaala wa elimu mbadala kwa wasichana na wavulana walioacha shule kwa sababu mbalimbali; na
vi. Kundaa na kutekeleza programu za kuzuia ukatili wa kijinsia kwa wavulana, wasichana, wanawake na wanaume katika taasisi za elimu.

**Shabaha**

i. Ushiriki wa wanawake na wasichana katika programu za elimu katika ngazi zote kuongezeka ifikapo 2033;
ii. Miundombinu rafiki na vifaa vya ujifunzaji kwa wavulana na wasichana kuimarishwa ifikapo 2033;
iii. Ushiriki wa wasichana katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) kuhamasishwa ifikapo 2033;
iv. Afua wezeshi za kuongeza idadi ya uandikishwaji ya wasichana na wavulana na kuhakikisha wanabakia shuleni kuandaliwa ifikapo 2033;
v. Afua wezeshi za kuongeza idadi ya uandikishwaji ya wasichana na wavulana na kuhakikisha wanabakia shuleni kutekelezwa ifikapo 2033;
vi. Elimu mbadala kwa wasichana na wavulana walioacha shule kwa sababu mbalimbali kutolewa ifikapo 2033;
vii. Programu za kuzuia ukatili wa kijinsia kwa wavulana, wasichana, wanawake na wanaume katika taasisi za elimu kuandaliwa ifikapo 2033; na
viii. Programu za kuzuia ukatili wa kijinsia kwa wavulana, wasichana, wanawake na wanaume katika taasisi za elimu zimeanza kutekelezwa ifikapo 2033.

### 3.2.6 Afya na Jinsia

**Lengo**

Kuboresha huduma jumuishaji za afya ikiwemo afya ya uzazi na magonjwa yasiyoambukiza kwa wanawake na wanaume.

**Mikakati**

i. Kuendeleza uingizaji wa masuala jinsia katika sera, programu, na mipango ya sekta ya afya;

ii. Kuendeleza ushiriki wa wanawake, wanaume, wasichana, na wavulana katika programu za afya ya uzazi na afya ya akili;
iii. Kuhamasisha kuzingatiwa kwa mtindo bora wa maisha yenye afya katika kukabiliana na changamoto za lishe kwa wanawake, wasichana, wanaume, na wavulana; na
iv. Kuwahimiza wanaume, wanawake, wasichana na wavulana kufanya uchunguzi wa afya mara kwa mara ili kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza ikiwa ni pamoja na saratani ya shingo ya kizazi na saratani ya tezi dume.

**Shabaha**

i. Uingizwaji wa masula ya  jinsia katika sera, programu, na mipango ya sekta ya afya kuzingatiwa ifikapo mwaka 2033;
ii. Ushiriki wa wanawake, wanaume, wasichana, na wavulana katika programu za afya ya uzazi na akili kuhimarishwa ifikapo mwaka 2033;
iii. Kuhimiza mtindo bora wa maisha ili kutatua changamoto za afya na lishe ifikapo mwaka 2033;
iv. Kuhimiza mtindo bora wa maisha ili kuzuia magonjwa yasiyoambukiza kwa wanawake, wasichana, wanaume, na wavulana ifikapo mwaka 2033.

### 3.2.7 Jinsia, Teknolojia na Ubunifu

**Lengo**

Kimarisha matumizi ya teknolojia ili kuwawezesha wanawake.

**Mikakati**

i. Kuanzisha na kuhimiza utekelezaji wa mifumo ya kisheria inayosimamia matumizi ya mtandao na majukwaa ya kijamii kwa lengo la kupambana na ukatili dhidi ya wanawake;
ii. Kuimiza matumizi chanya ya majukwaa ya kidijitali kwa lengo la kupambana na ukatili dhidi ya wanawake mtandaoni;
iii. Kuandaa mipango ya kuongeza uelewa wa wanawake kuhusu umuhimu wa teknolojia katika kuimarisha mnyororo wa thamani wa bidhaa;

iv. Kuandaa na kutekeleza ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi katika kukuza mipango ya kuimarisha upatikanaji wa teknolojia rahisi kutumika kwa watumiaji;
v. Kukuza uelewa kuhusu matumizi chanya ya teknolojia ya kidijitali na zisizo za kidijitali kwa wanawake na wanaume;
vi. Kuongeza matumizi ya mifumo ya kidijitali katika kupambana na ukatili wa kijinsia.

**Shabaha**

i. Majukwaa ya kidijitali yanayoonesha taswira chanya za wanawake, wanaume, wavulana, na wasichana kuanzishwa ifikapo mwaka 2033;
ii. Matukio ya ukatili dhidi ya wanawake mtandaoni kupunguzwa ifikapo mwaka 2033;
iii. Mipango ya kuongeza uelewa wa wanawake kuhusu umuhimu wa teknolojia katika kuimarisha mnyororo wa thamani wa bidhaa kuanzishwa ifikapo mwaka 2033;
iv. Ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) unaoendeleza mipango ya kuimarisha upatikanaji wa teknolojia rahisi kuimarishwa ifikapo mwaka 2033;
v. Ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) unaoendeleza mipango ya kuimarisha upatikanaji wa teknolojia rahisi kuimarishwa ifikapo mwaka 2033;
vi. Uelewa kuhusu matumizi chanya ya teknolojia za kidijitali na zisizo za kidijitali kwa wanawake na wanaume kuimarishwa ifikapo mwaka 2033;
vii. Matumizi ya mifumo ya kidijitali katika kupambana na ukatili wa kijinsia kuendelezwa ifikapo mwaka 2033.

### 3.2.8 Jinsia na Takwimu

**Lengo**

Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji, uhifadhi, na matumizi ya takwimu za kijinsia.

**Mikakati**

i. Kuandaa mifumo ya kukusanya, kuchakata, kuhifadhi, na kutumia takwimu zilizogawanywa kwa jinsia;
ii. Kuimarisha uwekezaji katika utafiti na maendeleo ya kijinsia; na

iii. Kuandaa na kutekeleza mpango wa kuweka viashiria vya kijinsia katika tafiti mbalimbali.

**Shabaha**

i. Mifumo ya kukusanya, kuchakata, kuhifadhi, na kutumia takwimu zilizogawanywa kwa jinsia kuanzishwa ifikapo mwaka 2033;
ii. Uwekezaji katika tafiti na maendeleo ya kijinsia kuimarishwa ifikapo mwaka 2033;
iii. Mpango wa uzingatiaji wa viashiria vya masula ya kijinsia katika tafiti mbalimbali kuandaliwa ifikapo mwaka 2033; na
iv. Mpango wa uzingatiaji wa viashiria vya masula ya kijinsia katika tafiti mbalimbali umetekelezwa ifikapo mwaka 2033.

### 3.2.9 Wanawake, Amani na Usalama

**Lengo**

Kuzingatia uingizwaji wa masuala ya kijinisa kwenye vyombo vya ulinzi na usalama na programu za amani.

**Mikakati**

i. Kuandaa na kutekeleza programu za kuongeza uelewa katika jamii kuhusu ajenda ya wanawake, amani, na usalama;
ii. Kuandaa na kutekeleza sera na mfumo wa kisheria wa kukuza mchango na ushiriki wa wanawake katika miundo ya usalama na mchakato wa amani;
iii. Kuandaa na kutekeleza mwongozo wa kushughulikia ukatili wa kijinsia wakati wa majanga na matukio ya migogoro;
iv. Kuandaa na kutekeleza programu za kushughulikia mahitaji ya kijinsia wakati wa kurejesha hali ya utulivu na amani baada ya migogoro na majanga ya asili.

**Shabaha**

(i) Programu za kuongeza uelewa katika jamii kuhusu ajenda ya wanawake, amani, na usalama kuandaliwa ifikapo mwaka 2033;
(ii) Programu za kuongeza uelewa katika jamii kuhusu ajenda ya wanawake, amani, na usalama kutekelezwa ifikapo mwaka 2033;

(iii) Sera na mfumo wa kisheria unaozingatia mchango na ushiriki wa wanawake katika miundo ya usalama na mchakato wa amani kuandaliwa ifikapo mwaka 2033;

(iv) Sera na mfumo wa kisheria unaozingatia mchango na ushiriki wa wanawake katika miundo ya usalama na mchakato wa amani kutekelezwa ifikapo mwaka 2033;

(v) Mwongozo wa kushughulikia ukatili wa kijinsia wakati wa majanga na migogoro kuandaliwa ifikapo mwaka 2033;

(vi) Mwongozo wa kushughulikia ukatili wa kijinsia wakati wa majanga na migogoro kutekelezwa ifikapo mwaka 2033;

(vii) Programu za kushughulikia mahitaji ya kijinsia wakati wa kurejesha hali ya utulivu na amani baada ya migogoro na majanga ya asili kuandaliwa ifikapo mwaka 2033; na

(viii) Programu za kushughulikia mahitaji ya kijinsia wakati wa kurejesha hali ya utulivu na amani baada ya migogoro na majanga ya asili kutekelezwa ifikapo mwaka 2033.

### 3.2.10 Jinsia na Utawala Bora

**Lengo**

Kuendeleza uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika kanuni za utawala bora.

**Mikakati**

i. Kuandaa na kutekeleza mipango ya kuimarisha uzingatiajia wa masuala ya jinsia katika kanuni za utawala bora;
ii. Kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuongeza uelewa katika jamii kuhusu kanuni za utawala bora zinazozingatia masuala ya kijinsia; na
iii. Kuingiza masuala ya kijinsia katika programu za utawala bora.

**Shabaha**

i. Mipango ya kuimarisha uzingatiajia wa masuala ya jinsia katika kanuni za utawala bora kuandaliwa ifikapo 2033;
ii. Mipango ya kuimarisha uzingatiajia wa masuala ya jinsia katika kanuni za utawala bora kutekelezwa ifikapo 2033;

iii. Mikakati ya kuongeza uelewa katika jamii kuhusu kanuni za utawala bora zinazozingatia masuala ya kijinsia kuandaliwa ifikapo 2033;
iv. Mikakati ya kuongeza uelewa katika jamii kuhusu kanuni za utawala bora zinazozingatia masuala ya kijinsia kutekelezwa ifikapo 2033; na
v. Kuimarisha uingizaji wa masuala ya kijinsia katika programu za utawala bora ifikapo 2033.

### 3.2.11 Jinsia na VVU na Ukimwi

**Lengo**

Kuimarisha ufuasi wa utoaji wa huduma kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI, pamoja na kuzuia maambukizi mapya ya VVU kati ya wanaume na wanawake.

**Mikakati**

i. Kuandaa na kutekeleza programu za kuongeza uelewa kuhusu athari za VVU/UKIMWI na unyanyapaa kwa wanawake, wanaume, wasichana, na wavulana; na
ii. Kuunda mazingira wezeshi yanayowezesha wanawake, wanaume, wasichana, na wavulana kupata huduma za VVU/UKIMWI, vipimo vya hiari, na kufuata matibabu.

**Shabaha**

i. Programu za kuongeza uelewa kuhusu athari za VVU/UKIMWI na unyanyapaa kwa wanawake, wanaume, wasichana, na wavulana kuandaliwa ifikapo mwaka 2033;
ii. Programu za kuongeza uelewa kuhusu athari za VVU/UKIMWI na unyanyapaa kwa wanawake, wanaume, wasichana, na wavulana kutekelezwa ifikapo mwaka 2033; na
iii. Kuweka mazingira wezeshi kwa wanawake, wanaume, wasichana, na wavulana kupata huduma za VVU/UKIMWI, vipimo vya hiari, na ufuasi mzuri wa matibabu kuandaliwa ifikapo mwaka 2033.

### 3.2.12 Jinsia na Mazingira

**Lengo**

Kuimarisha uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika usimamizi wa mazingira.

**Mikakati**

i. Kuandaa programu za kijinsia za kuongeza uelewa kuhusu uhifadhi wa mazingira; na
ii. Kuimarisha uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika programu za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

**Shabaha**

i. Programu za kijinsia za kuongeza uelewa kuhusu uhifadhi wa mazingira kuandaliwa ifikapo 2033;
ii. Programu za kijinsia za kuongeza uelewa kuhusu uhifadhi wa mazingira kutekelezwa ifikapo 2033; na
iii. Uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika programu za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa kuimarishwa ifikapo 2033.

## SURA YA NNE

## UFUATILIAJI NA TATHMINI

### 4.1 Utangulizi

Ufuatiliaji na tathmini ni kipengele muhimu katika utekelezaji wa Sera (2023). Kwa kuzingatia kwamba masuala ya jinsia ni mtambuka na yanahusisha sekta mbalimbali, ufuatiliaji na tathmini utafanyika kupitia Wizara mbalimbali, Idara, Wakala za Serikali, Mashirika, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, AZAKI, Wadau wa Maendeleo, Sekta binafsi na Jamii . Aidha, Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum itaratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera hii katika ngazi ya Taifa.

Ufuatiliaji na tathmini utahusisha kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini, kukusanya taarifa za awali za jinsia za kisekta zitakazotumika kufuatilia utekelezaji wa malengo katika kila eneo la sera. Ufuatiliaji na Tathimini wa utekelezaji wa Sera (2023) utafanyika kwa vipindi vya robo mwaka, nusu mwaka na katika kipindi cha mwaka mmoja ili kupima matokeo ya utekelezaji kulingana na shabaha zilizowekwa.Aidha, tathmini itahusisha kupitia taarifa mbalimbali za utafiti na kupata maoni kutoka kwa walengwa wa sera ili kubaini juhudi za ufanisi, mipango, programu, mikakati na ufanisi wa rasilimali katika kufikia malengo na kufikia matokeo yaliyokusudiwa. Ufuatiliaji na Tathmini utazingatia maeneo yafuatayo: **-**

(i) Kuwaongoza wadau kutekeleza afua za kisera kwa kuzingatia mipango, programu, na mikakati ya wizara za sekta, wakala mbalimbali na kuandaa viashiria vya matokeo vinavyozingatia jinsia kwa watu binafsi, kaya na jamii;

(ii) Kuimarisha ushirikiano na AZAKI ili kubaini maeneo ya vipaumbele vya kila shirika na hivyo kuondoa mwingiliano wa majukumu;

(iii) Kuandaa viashiria vya kijamii vya kupima usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake;

(iv) Kuandaa viashiria vinavyozingatia usawa wa kijinsia na umaskini katika ngazi ya mtu binafsi, familia, utawala na kwa jamii kwa ujumla;

(v) Kuwezesha kufanyika kwa uratibu na tathmini ya kina ya mfumo wa matokeo ya jitihada na afua za uingizaji wa masuala ya kijinsia kuendana na mikakakati ya Sera;

(vi) Kuongeza ushiriki wa jamii katika muundo wa uongozi wa programu za ulinzi na ustawi wa jamii ili kuipajamii uwezo wa kuwajibisha mamlaka husika;

(vii) Kutathmini miradi yote ya ulinzi na ustawi wa jamii na programu ili kubaini kama zinaendana na shabaha za sera na matarajio ya kufikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake;

(viii) Kuweka kumbukumbu za taarifa na takwimu mbalimbali kuhusu masuala ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake; na

(ix) Kutathmini utoshelevu wa rasilimali na mgao wa kibajeti katika shabaha zilipangwa.

## 4.2 Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini

Mkakati wa ufuatiliaji na tathmini unahusisha:-

(i) Kukusanya taarifa za kila mwezi kutoka kwa taasisi zote zinazotekeleza mikakati ya sera hii;

(ii) Kufanya ufuatiliaji wa kila mwaka na ukaguzi wa ubora wa huduma zinazotolewa katika jamii; na

(iii) Kufanya mapitio ya kila mwaka ya utekelezaji wa sera pamoja na tathmini ya uwezo wa kitaasisi.

## 4.3 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini unalenga kutoa mwongozo wa utekelezaji wa Sera na mkakati wa utekelezaji wake. Muundo unaainisha yafuatayo:

(i) Viashiria vya utendaji kwa ajili ya tathmini ya sera na programu;

(i) Shabaha na mikakati ya utekelezaji wa sera; na

(ii) Kuongoza ushiriki wa wadau katika utekelezaji na ufuatiliaji wa shughuli.

Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini umejumuisha uchambuzi wa malengo, mikakati, shabaha, viashiria vya utendaji, kizio(baseline), vyanzo vya taarifa na takwimu, njia ya kuthibitisha (means of verification) pamoja na wahusika . Aidha bango kitita la Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini limeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.1**.

### 4.4 Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji utahusisha ukusanyaji endelevu wa taarifa na takwimu, uchambuzi, upimaji wa viashiria na kutoa taarifa za matokeo ya uchambuzi. Hii itatoa taarifa kwa wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na wadau kuhusu afua zinazoendelea kutekelezwa, kwa madhumuni ya kutathmini mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojitokeza ili kuchukua hatua stahiki za kuboresha utendaji.

#### 4.4.1 Mawanda ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Mfumo wa ufuatiliaji na tathimini unashughulikia maeneo yafuatayo:

(i) Upimaji wa vitendanishi (input),Shughuli, matokeo ya muda mfupi, matokeo ya muda wa kati na malengo;

(ii) Kanzidata ya kuhifadhi taarifa na takwimu unaotumika na Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ; na

(iii) Mpango wa utekelezaji wa ufuatiliaji.

#### 4.4.2 Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini

Mfumo wa ufuatiliaji na tathimini wa utekelezaji wa sera utazingatia yafuatayo:

(i) Kuunganisha mfumo wa ufuatiliaji na tathimini na mifumo mingine ya serikali;

(ii) Utumiaji wa mfumo wa usimamizi unaozingatia matokeo;

(iii) Kuanzisha programu za kuwajengea uwezo watekelezaji wa ufuatiliaji na tathmini; na

(iv) Kufanya mapitio ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini.

### 4.5 Mpango wa utoaji taarifa ya utendaji kazi

Mpango huu utahusisha utoaji wa taarifa za utendaji kazi kwa kuzingatia Malengo na Shabaha ya Sera. Mpango utahusisha utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Shabaha dhidi ya matumizi ya rasilimali zinazolenga kuleta matokeo chanya yaliyotalajiwa kuifikia jamii na wa wadau kwa ujumla. Vilevile, Mpango utahusisha utoaji wa taarifa ndani na nje ya taasisi.

#### 4.5.1 Mpango wa Taarifa ya Ndani

Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalaum itawajibika kuandaa taarifa za ndani za utendaji zinazohusu maendeleo yaliyofikiwa kwa kila wiki, mwezi, robo mwaka nusu mwaka na mwaka. Pia wizara

kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itafanya tathmini ya utekelezaji wa Sera na kutoa taarifa za tathmini za muhula wa kati na wa mwisho. Taarifa hizi zitawasilishwa kwenye Menejimenti ya Wizara ili kutoa mwongozo wa kufanya maamuzi yenye lengo la kuboresha utekelezaji ili kufikia Malengo ya Sera (2023) kama ilivyo onyesha katika **Jedwali Na. 1**.

**Jedwali Na. 1**: Utoaji wa taarifa za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera (2023)

| Na. | Aina ya Taarifa | Mpokeaji wa Taarifa | Muda wa utoaji taarifa | Muhusika |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Taarifa za Idara/Vitengo | Katibu Mkuu | Kila wiki | Wakurugenzi wa Idara na Vitengo/Wakuu wa Vitengo na Taasisi |
| 2. | Taarifa ya utekelezaji ya robo mwaka | Katibu Mkuu | Robo mwaka | Wakurugenzi wa Idara na Vitengo/Wakuu wa Vitengo na Taasisi |
| 3. | Taarifa ya utekelezaji ya nusu mwaka | Katibu Mkuu | Nusu mwaka | Wakurugenzi wa Idara na Vitengo/Wakuu wa Vitengo na Taasisi |
| 4. | Taarifa ya utekelezaji ya mwaka | Katibu Mkuu | Kila mwaka | Wakurugenzi wa Idara na Vitengo/Wakuu wa Vitengo na Taasisi |
| 5. | Taarifa ya Tathmini | Katibu Mkuu | Taarifa ya nusu mhula (Mid-term) | Wakurugenzi wa Idara na Vitengo/Wakuu wa Vitengo na Taasisi |
| 6. | Taarifa ya Tathmini | Katibu Mkuu | Taarifa ya mhula (End-term) | Wakurugenzi wa Idara na Vitengo/Wakuu wa Vitengo na Taasisi |

### 4.5.2 Mpango wa Utoaji wa Taarifa kwa Wadau wa Nje ya Wizara

Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalaum itakuwa na jukumu la kuandaa na kusambaza taarifa za utendaji wa sera kwa matumizi ya nje.Taarifa hizo zitawasilishwa kwa wadau wa nje ya wizara kama vile Wizara za Kisekta, Idara na Taasisi za Serikali zianazo jitegemea, Bunge,Wadau wa Maendeleo, Asasi za Kiraia na Umma kwa ujumla.

### 4.5.3 Matumizi ya taarifa za Ufuatiliaji na Tathimini.

Taarifa za Ufuatiliaji na Tathimini  zitaiinufaisha Wizara za Kisekta, Idara na Taasisi

za Serikali zinazo jitegemea, Bunge,Wadau wa Maendeleo, Asasi za Kiraia na Umma katika muktadha wa:

(i) Kuboresha utoaji wa huduma;

(ii) Kuimarisha uwajibikaji; na

(iii) Kufanya maamuzi,

(iv) Kuandaa Mipango; na

(v) Kutenga rasilimali zinazohitajika katika utekelezaji wa sera.

**KIAMBATISHO 1:**

## BANGO KITITA LA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA SERA YA TAIFA YA JINSIA NA MAENDELEO YA WANAWAKE (2023)

| LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | SERIKALI (000,000) | WADAU WA MAENDELEO (000,000) | JUMLA RASILIMALI (000,000) | MUDA | NAMNA YA KUTHIBITISHA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Eneo la Sera 1: Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi** | | | | | | | | | |
| Kuimarisha usawa wa kjinsia katika upatikanaji wa fursa za kiuchumi na mitaji kwa wanawake na wanaume. | Kuchukua hatua za kupunguza mkwamo na kupanua upatikanaji wa rasilimali za mitaji kwa wanawake ili kuongeza uzalishaji. | Kuhakikisha ongezeko la wanawake wanaopata mitaji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi ifikapo Juni, 2033 | Idadi ya wanawake waliopata mitaji | 800 | 800 | **1,600** | 2032 | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | WMJJWM, NEEC, SIDO, BoT, OR-TAMISEMI & TPSF |
| | | | Idadi ya Taasisi zinazotoa mitaji (mikopo yenye masharti nafuu, mitaji ya kianzio) kwa wanawake wajasiriamali | | | | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | WMJJWM, NEEC, SIDO, BoT, OR-TAMISEMI & TPSF |
| | | | Idadi ya biashara ndogo na za kati (SMEs) zinazomilikiwa na wanawake | | | | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | NEEC, BRELA & TPSF |
| | | | Idadi ya shughuli za wanawake za kujipatia kipato zilizowezeshwa kwa kupatiwa mitaji | | | | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | OWM - KAZI, WMJJWM, NEEC, SIDO, MoF, BoT, OR-TAMISEMI & TPSF |
| | | | Idadi ya vikundi vya wanawake vya kiuchumi vilivyoanzishwa | | | | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | BoT & OR-TAMISEMI |
| | | | Thamani ya mitaji iliyotolewa kwa wanawake | | | | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | OWM-KAZI, WMJJWM, NEEC, SIDO, MoF, BoT, OR-TAMISEMI & TPSF |
| | Kubainisha na kutekeleza jitihada zenye lengo la kuwawezesha wanaume na wanawake kutambua na kutumia fursa za | Jitihada za kuwezesha wanaume na wanawake kutambua na kutekeleza fursa za kiuchumi | Idadi ya jitihada zilizotekelezwa kwa ajili ya kuwawezesha wanawake na wanaume kunufaika na fursa za kiuchumi | 800 | 800 | **1,600** | 2032 | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | NEEC, PMO- LYED |
| | | | Uwiano (proportion) wa | | | | | Taarifa za tafiti za Taifa, | NEEC & MDAs |

| LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | SERIKALI (000,000) | WADAU WA MAENDELEO (000,000) | JUMLA RASILIMALI (000,000) | MUDA | NAMNA YA KUTHIBITISHA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | kiuchumi | ifikapo Juni, 2033 | wanawake walionufaika na fursa za kiuchumi | | | | | Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | |
| | Kushawishi kuzingatiwa kwa mgawanyo na upangaji wa majukumu ya kazi za nyumbani na majukumu ya malezi kati ya wanaume na wanawake kwa kuzingatia usawa; | Kuwepo kwa mgawanyo sawa wa majukumu ya kazi za nyumbani na malezi kati ya wanaume na wanawake ifikapo Juni, 2033 | Uwiano wa muda unaotumika na wanawake kwa shughuliza za nyumbani na malezi ya familia alionufaika na fursa za kiuchumi | 700 | 700 | **1,400** | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | NBS & MCDGWSG |
| | Kuendeleza na kuimarisha ushiriki wa wadau katika kusaidia kufanya mabadiliko ya kijamii yenye maadili chanya; | Ushirikishwaji wa wadau katika kukuza mabadiliko chanya ya mila na maadili ya kijamii kuimarishwa ifikapo Juni, 2028 | Uwiano wa wanawake wanaoathiriwa na mila zenye kuleta madhara (kama vile, Ukeketaji na ndoa za utotoni) | 800 | 800 | **1,600** | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | NBS & MCDGWSG |
| | | | Uwiano wa idadi ya watu wanaohamasisha mila na desturi chanya katika jamii | | | | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | NBS & MCDGWSG |
| | | | Idadi ya wadau wanaohamasisha kupinga mila na desturi zenye kuleta madhara | | | | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | WMJJWM & Wizara ya Michezo na Utamaduni |
| | Kuhimiza umuhimu wa kujiunga katika programu za hifadhi ya jamii kwa wanawake na wanaume, wafanyakazi wa sekta binafsi na sekta za umma wanaoishi mijini na vijijini. | Upatikanaji na usambazaji wa huduma za usalama wa jamii kwa wafanyakazi katika sekta binafsi na sekta za umma kwa wanawake na wanaume wanaoishi mijini | Idadi ya programu za hifadhi ya jamii iliyopo | 800 | 800 | **1,600** | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | OWM-KAZI & MoF |
| | | | Uwiano wa idadi ya watu katika sekta isiyo rasmi waliojiandikisha kwenye programu za hifadhi ya jamii | | | | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | OWM-KAZI & MoF |

| LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | SERIKALI (000,000) | WADAU WA MAENDELEO (000,000) | JUMLA RASILIMALI (000,000) | MUDA | NAMNA YA KUTHIBITISHA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | na vijijini kuimarishwa ifikapo Juni, 2028. | | | | | | | |
| **JUMLA NDOGO** | | | | **3,900** | **3,900** | **7,800** | | | |
| | | | | | | | | | |
| **Eneo la Sera 2: Ukatili wa Kijinsia** | | | | | | | | | |
| Kutokomeza aina zote za ukatili wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na ukatili wa kijinsia mtandaoni. | Kuandaa programu za kuongeza uelewa mtandaoni kuhusu kuzuia na kushughulikia ukatili wa kijinsia mtandaoni; | Matukio ya ukatili wa kijinsia kupungua ifikapo 2028 | Idadi ya programu za kutokomeza ukatili wa kijinsia | 700 | 700 | **1,400** | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | WMJJWM & Wizara za Kisekta |
| | | | Uwiano wa wanawake waliofanyiwa ukatili wa kijinsia (Ukatili wa kingono, kimwili, kisaikolojia, kiuchumi na kimtandao) | | | | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | NBS, OR-TAMISEMI, MoHA |
| | | | Idadi ya za kesi za ukatili wa kijinsia (GBV) zilizoripotiwa | | | | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | MoHA & MoCLA |
| | | | Uwiano wa idadi ya watu walioathirika na ukatili wa kijinsia kwa umri na jinsi (Kingono, Kimwili, Kisaikolojia, Kiuchumi, Mtandaoni) | | | | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | NBS, OR-TAMISEMI, MoHA |
| | Kuimarisha mifumo ya uratibu kwa ajili ya kuzuia na kushughulikia ukatili wa kijinsia katika jamii; | Mifumo ya uratibu kwa ajili ya kuzuia na kushughulikia ukatili wa kijinsia katika jamii kuimarishwa ifikapo 2028; | Uwepo kwa mfumo madhubuti wa kuratibu kuzuia na kushughulikia ukatili wa kijinsia (GBV) | 800 | 800 | **1,600** | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | WMJJWM, OWM-KAZI & OR-TAMISEMI |
| | | | Idadi ya mifumo ya kijamii ya kuratibu kuzuia na kushughulikia ukatili wa kijinsia | | | | | Taarifa za tafiti za Taifa, Taarifa za utekelezaji za robo, nusu na mwaka; na Hotuba za Bajeti | WMJJWM, OWM-KAZI & OR-TAMISEMI |
